# JARIDA LA ATD DUNIA YA NNE TANZANIA

Aprili 2018

"Popote pale wanaume kwa wanawake wanapolazimika kuishi katika maisha ya umaskini uliokithiri, haki za binadamu hukiukwa. Sote ni wajibu wetu wa dhati kujiunga pamoja na kuhakikisha kwamba haki hizi zinaheshimika".

- Joseph Wresinski (1917-1988), founder of ATD Fourth World -

## Tahariri



Hili ni jarida la kwanza kwa mwaka huu wa 2018. Tunayo furaha kushirikishana nanyi habari tukitumaini kwamba mnaendelea vema mkiwa na nguvu katika majukumu yenu ya kila siku.

Kwa upande wetu tunaendelea vizuri. Tulikuwa na fursa ya kukaribisha watu mbalimbali ambao walijiunga na kusaidiana nasi katika mambo kadhaa: Bwana Bruno Dabout mmoja kati ya timu ya uongozi wa kimataifa ya ATD, Bwana Martin Kalisa kutoka katika uongozi wa kanda ya Afrika, marafiki kutoka Kilimanjaro, Mbeya, Njombe, Dodoma na kadhalika….wote walishiriki pamoja nasi mnamo mwezi March katika tukio maalumu. Walishiriki kwa ukamilifu katika mikutano pia walikuwa msaada mkubwa katika kufaniksha jukumu letu.
Kwa ukamilfu kama ilivyokuwa imetaarifiwa katika jarida letu la mwishoni mwa mwaka 2017, tumehitimisha mradi wa Elimu kwa Wote kwa kuratibu semina ya kitaifa mwezi wa march 2018: Familia pamoja na watu mbalimbali tulikutana pamoja na kushirikisha namna walivyojitolea katika mradi. Washiriki walionesha hitimisho lao la jumla jinsi ilivyo muhimu kuwepo ushirikiano sawa katika kufikia mafanikio ya watoto shuleni. Tarehe 2 ya mwezi Juni, wafanyakazi wa kujitolea pamoja na marafiki watakuhudhuria katika semina ya kimataifa itakayofanyika Pierrelaye, makao makuu ya shirika ambapo shuhuda za elimu kwa wote zitatuwezesha kuelewa tulichojifunza kutokana na mafanikio ya mradi huu.
Utafiti wa vipimo vya umaskini unaendelea. Tumeanza kukutana na watu nje ya Dar-es-salaam katika mkoa wa Dodoma vijijini hususan katika wilaya za Kondoa na Bahi. Utafiti huu umetuonesha kwamba hadi sasa haki za binadamu hasa kwa walio maskini bado zinakiukwa. Wakati mwingine mazingira duni hufanya hali kuwa mbaya zaidi. Kila mmoja wetu ameshuhudia majanga yaliyosababishwa na mvua kubwa mwezi uliopita ambapo idadi ya nyumba nyingi ziliathirika kwa mafuriko na baadhi ya watu kupoteza maisha na bado watu wengi wanataabika.
Tunatarajia kusonga mbele katika utafiti kwa kukutana na watu wa Njombe hivi karibuni.
Haya ndiyo majukumu makubwa ambayo timu ilikuwa imelenga kuyatekeleza kipindi hiki. Tunawatakia heri wote. Wapeni moyo wale wote ambao wamepata athari kutokana na mvua hizi kubwa. Kwa pamoja tunaweza kuleta mabadiliko.

Alexie Gasengayire, ATD Volunteer
Mwana katika Timu ya Uongozi.



## Katika kijiji cha Bahi

Kupitia mradi wa utafiti wa vipimo vya umaskini, ugunduzi wa maisha ya vijijini katika eneo la Dodoma : wilaya za Bahi na Kondoa.

Hatua ifuatayo ya utafiti shirikishi ilikuwa kukutana na jumuiya za vijijini : kwa jarida hili tulitaka kushilikishana nanyi kuhusu wilaya ya Bahi. Kwa uhalisia wilaya ya Bahi ni moja wapo kati ya wilaya saba za mkoa wa Dodoma. Uchumi wa Bahi unategemea kilimo (mazao na mifugo). Hata hivyo wilaya hii inakabiliwa na msimu mrefu wa ukame. Maji ni changamoto kubwa. Utafiti wetu ulifanyika katika kijiji cha Nkhome, katika kata ya Ibugule ambapo tulikutana na wanaume na wanawake wanaotoka kwenye maisha ya aina mbalimbali. Hii iliwezekana kwa msaada mkubwa wa rafiki yetu Peter Msasu. Wenyeji wa kijiji hiki wengi asili yao ni Wagogo.

Tulishangazwa na ujasiri mkubwa wa wenyeji, kutokana na hali kwamba watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri wanakabiliana na changamoto zile zile pia matatizo yale yale, wao wenyewe wamejijengea aina ya ushirikiano ili kuweza kushirikiana na kusaidiana wao kwa wao. Kama vile katika kulima ambapo husaidiana kulima mashamba yao kwa zamu. Kwa mfano huu hii huwasaidia kupanda mazao kwa msimu.

Tulijifunza mengi kutokana na mifano hii. Ushirikiano miongoni mwa watu ni thamani kubwa katika kupambana na umaskini na kuboresha umoja katika jumuiya. Katika jarida lifuatalo tutaeleza mengi kuhusiana na tuliyojifunza kutokana na utafiti huu wa kubaini vipimo vya umaskini. .

Tarehe 6 mwezi wa Machi tulikuwa na semina ya Elimu kwa Wote kushea matokeo tuliyo yapata kipindi cha utambulisho wa mapendekezo tuliyofanya shule 14 tofauti tofauti dar es Salaam na mikoa ya nje ya Dar es Salaam.

Lengo na dhumuni la hii semina tulifikiria ni muhimu sana kuwaleta pamoja walimu, maafisa elimu tuliokutananao kipindi cha utambulisho wa mapendekezo katika shule zao na washikadau wengine kuwashirikisha na wao jinsi gani mapendekezo yameleta mabadiliko kwenye shule zao. Hakika wakati huu ulikuwa ni muhimu sana kwa sababu uliwaleta pamoja walimu, maafisa elimu, wazazi, mashirika tofauti tofauti na washikadau wengine wa elimu na walisikia kitu gani walikishuhudia baada ya mawasilisho katika shule zao.

Matokeo baada ya mkutano na wazazi, walimu na timu ya uwasilishaji ya ATD Dunia ya Nne katika shule ya msingi Mwereni iliyopo Moshi Mkoani Kilimanjaro, uliwasaidia wazazi kuwa na muitikio chanya na kuhudhuria shughuli mbalimbali za shule pia kushiriki katika mikutano yote ya shule na kufuatilia maendeleo ya shule kwa watoto wao.

Hivyo muitikio huu uliwawezesha kupata maendeleo mazuri kitaaluma na kuwa na matokeo mazuri kwa sababu wazazi wanawasimamia vizuri na hivyo kupungua sana utoro shuleni kwa watoto wa kutokwenda shule. Na sasa mahudhurio ya watoto shuleni ni mazuri sana na wanajifunza kwa bidi, mahudhurio ya wazazi katika mikutano ya shule ni mazuri sana ukilinganisha na kipindi cha nyuma kabla ya Mkutano na Timu ya Uwasilishaji mapendekezo ya ATD Dunia ya Nne.

## Chakula mashuleni,

Hata hivyo, katika kikao hicho kulishauriwa wanafunzi kupata chakula cha mchana shuleni, hivyo shule yetu inaendelea kutoa huduma ya chakula cha mchana shuleni, huduma hii ya chakula imepelelekea wanafunzi kusoma kwa ufanisi mkubwa na kuweza kufanya vizuri katika masomo yao. Hivyo Shule mbili zilizopo nje ya Dar es Salaam zimeanza kutoa huduma za chakula kwa wanafunzi shule hizo ni shule ya msingi Mwerereni iliyopo Moshi Mkoani Kilimanjaro na shule ya Msingi Mkiu iliyopo Mkoa wa Njombe . Kutokana na agizo la serikali kuhusu elimu bila malipo, jumuiya ya wazazi imeandaa kamati maalum ya kusimamia chakula ambayo inaongozwa na wazazi wenyewe. Chakula hiki kimekuwepo kwa wanafunzi wote wa kutwa na wabweni, aidha wanafunzi wanaotoka katika mazingira magumu ambao wanashindwa kuchangia chakula wanasaidiwa kutokana na wale wanaochangia hivyo upata chakula bila kubaguliwa. Vilevile kutokana na kikao cha tarehe 22/02/2018 wamekubaliana kwa pamoja kuunda na kuanzisha mfuko wa wazazi kwa ajili ya kugharamia chakula na masomo ya zida kutoka kwa wadau mbali mbali wa elimu.

Matokeo haya chanya wadau na mashirika mbalimbali walioshiriki kwenye semina walisema kwamba mbinu hii ya kuanzisha mfuko wa wazazi ni mzuri na shule nyingine ziige ili kuborehsa elimu kwa watoto wetu kwani mtoto mwenye njaa kamwe hawezi kujifunza.

Na Mwalimu Mkuu kutoka shule ya msingi Tandale alisema, “baadhi ya wazazi kipindi cha nyuma hawakujua umuhimu wa elimu, baada ya Shirika la ATD Dunia ya Nne kuandaa mkutano na walimu na wazazi na kuwashirikisha maarifa wameanza kutambua umuhimu wa elimu. Hivi sasa wameanza kuwapeleka watoto wao shule ingawa wao wenyewe hawajui kusoma na kuandika. ATD Dunia ya Nne ilianzisha darasa la elimu ya watu wazima kwenye shule yetu ya msingi Tandale na wazazi wanashiriki katika darasa hilo kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili ili angalau waweze kukagua madaftari ya watoto wao wanapotoka shuleni. Baada ya ATD kumaliza programu yao ya miezi Mitatu ya darasa la elimu ya watu wazima, uongozi wa shule ya msingi Tandale waliamua kuendelea na programu hii ya darasa la elimu ya watu wazima na mpaka sasa darasa linaendelea katika shule ya msingi Tandale.




Decemba 2017

**SEMINA YA VIJANA**

"Kuwezesha maktaba ya mtaani"

Mbagala, Dar es Salaam

Mwaka jana mwezi Desemba, ATD Dunia ya Nne iliandaa semina ya vijana ya juma moja, iliyofanyika katika Monesteri ya Watawa wa kike wa Benedektini kule Mbagala. Semina hii iliwaleta pamoja vijana marafiki wa ATD kutoka jijini Dar es Salaam.

Lengo la semina hii lilikuwa kuimarisha jumuyia ya vijana wa ATD. Hawa ni vijana waliokuwa wamejitoa kufanya shughuli mbali mbali katika jamii na kujifunza kutoka kwa watu waliokuwa wakifanya au kukutana nao kikazi maana ya kuwa rafiki wa ATD. Moja wapo ya mambo ambayo wengi wao waliyataja yalikuwa umuhimu wa kujitoa na kuwa katibu na watu walioathirika na umaskini. Ilikuwa jambo kubwa sana kuwaona vijana hawa walivyojichukulia wenyewe kujipa majukumu haya hasa kama vijana katika jamii. Wakati huo huo tulitambua kwamba walikuwa wanakabiliana na changamoto mbali mbali katika shughuli walizokuwa wakifanya.

Hii semina ilitupatia fursa ya kuelewa changamoto wanazokabiliana nazo wanapowezesha maktaba ya mtaa. Maktaba ya mtaa ni mahali ambapo wawezeshaji wa ATD hukutana na watoto wakifanya shughuli mbali mbali. Kwa mfano katika maeneo jirani ya Tandale, lengo la maktaba ya mtaa ni kuwaleta pamoja watoto na kuimarisha uhusiano miongoni mwao, hususan pamoja na familia zao. Hata hivyo tulijifunza kwamba wakati vijana wa ATD wanapofanya kazi peke yao siyo kila mmoja katika jamii anayewachukulia vizuri au kukubaliana na matendo yao.

**Shafii, mmoja wa hawa wawezeshaji vijana wa ATD aligusia kwamba kuwezesha maktaba ya mtaani halikuwa jukumu rahisi.** Unalazimika kufikiria ni watoto gani wanahitaji kuangaliwa kwa karibu zaidi na namna ya kuhamasisha urafiki miongoni mwao. Mwezeshaji mwingine wa maktaba ya mtaani; Bahati alisisitiza kwamba kikundi kinatakiwaa kiratibiwe vizuri kuhakikisha kwamba watoto wote wanashiriki katika maktaba ya mtaa.

Baada ya kujifunza kuhusu maisha ya mhasisi wa ATD, Khalfani alisema, "Joseph Wresinski alijitoa kuishi mahali ambapo wengine walishindwa. Hakutaka watu waendelee kupokea misaada. Alitaka watu wasimame wenyewe; siyo kutegemea misaada. hakutaka watu wapoteze matumaini."

Kwa kushiriki kwao katika semina hii vijana waliweza kuelewa vizuri jinsi ya kukabiliana na changamoto wanazokabiliana nazo na kusonga mbele wakiwa na mtazamo hasi. Kuongezea, waliweza kuelewa kwa uwazi zaidi malengo ya jumla ya maktaba ya mtaa.

Mwisho, semina hii ilikuwa imeandaliwa ili kuwasaidia vijana kupata ufahamu zaidi kuhusu falsafa na maono ya muasisi wa ATD Joseph Wresinsky. Vijana wanalo jukumu kubwa katika kuchangia katika mapambano dhidi ya umaskini uliokithiri na wanatakiwa watambue kwamba wanalo jukumu katika shirika hili licha ya mazingira yao ya maisha.

Haki zetu ziko mikononi mwetu, ni wajibu wetu kuzifanya ziwe halisi MacDonald

Mack Donald

# Mrejesho wa siku ya. Tarehe 6 March 2018

Semina ya Elimu kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi kwa watoto wanaoishi katika Umaskini Uliokithiri ilifanyika katika Kituo cha utamaduni cha Ufaransa (Aliance France) Dar es salaam ikiwaleta pamoja wawakilishi wa mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Baada ya miaka miwili ya utafiti, mikutano na kushirikishana kila mdau aliweza kusikiliza na kujifunza kutoka kwa mwenzake. Tulisikia uwezekano wa mafanikio ya mazungumzo kati ya wazazi, walimu na wadau wote wa elimu. Tulijifunza mikakati ya kutokumwacha nyuma mtoto ye yote katika kupata elimu ya msingi na uwezekano maridhawa wa kujifunza shuleni. Tulijifunza jinsi tunavyofanikiwa tunapobadili mwelekeo kutoka katika hali ambayo kila mmoja husema “Ninafanya bidii” kuelekea pale tunaposema kwa pamoja, ”Tunaunganisha juhudi zetu”.



**Mkutano kati ya wana-ATD Dunia ya Nne, Bruno Dabout uongozi wa ATD Kimataifa, Martin Kalisa, Mmoja wa viongozi katika kanda ya Afrika, wajumbe kutoka wilaya za Mbeya, Moshi, Njombe na Dodoma. Kabla ya semina.**



**Wasanii walitumwiza siku. Shukrani kwa muziki na sauti za Kikundi cha Jitambue (Abdu Macha, Maru Mshana, Irene Erick).**



**Bibi Teddy, (Rosi Ubwe) kutoka Tandale, mwanakikundi wa kikundi cha uratibu cha Elimu kwa wote.**



**Zaidi ya watu 80 walishirikishana uzoefu wao wa utekelezaji wa mapendekezo ya Elimu kwa Wote yakiainisha mazingira sahihi ya kuungana pamoja kama uthibitisho wa mafanikio.**


ATD Dunia ya Nne - SLP 61786 - Dar es Salaam
Namba ya Ofisi: 0222761717
atd.tanzania@gmail.com
Kiswahili website: http://www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/tanzania/
Ukurasa wa Facebook: https://www.facebook.com/atd.duniayanne